1. YESU ANIONA

1. Nilivyotangatanga vyanitosha,
Sasa kwa Mungu wangu nirejee,
Chini yake Mwokozi najiinamisha,
Ili nikae kwake daima.

Na Yesu wangu aniona,
Rafiki mwema anipenda. X2

2. Njia ni wewe basi Yesu wangu,
Na kweli na uzima wa milele,
Mtu haji kwa Baba ila kwako,
Kwani wewe ni nuru ya dunia.

3. Nyumbani mwa Baba tuna makao,
Yesu alienda kutuandalia,
Tena atakuja kutuchukua,
Atupeleke kwetu mbinguni

4. Heri ni jina lake Mwokozi,
Kwani hakuna jina lingine kuu,
Nitalihofu jina lako kuu,
Nisikukasirishe Mungu wangu.

Na Yesu wangu aniona,
Rafiki mwema anipenda. X5

2. NILIPOTEA

1. Nilipotea sana dhambini,
Sikupata mtu wakuniongoza,
Lakini Yesu ndiye alinihurumia,
Akaniokoa, akanibadilisha.

Sasa yule mtu wa kwanza amepita,
Sasa mimi kiuumbe kipya ndani ya Yesu,
Nashukuru Mwokozi kwa neema yake,
Nilipo-potea yeye alinipata,
Nilipo-potea yeye alinipata.

2. Hili ni agano nitakaloagana,
Nao baada ya siku zile, anena Bwana,
Nitatia sheria zangu mioyoni mwao,
Na katika nia zao nitaziandika.

3. Dhabihu na toleo hukutaka,
Lakini mwili uliniwekea tayari,
Sadaka za kuteketezwa hukupendezwa,
Nimekuja niyafanye mapenzi yako.

Sasa yule mtu wa kwanza amepita,
Sasa mimi kiuumbe kipya ndani ya Yesu,
Nashukuru Mwokozi kwa neema yake,
Nilipo-potea yeye alinipata,
Nilipo-potea yeye alinipata. x2

3. OKOLEWA

1. Mwokozi Yesu anawaita,
Wenye kulemewa na wasumbukao,
Mje kwake Yesu awapumzishe,
Kila shida zote atazichukua.

Okolewa – atakupumzisha
Okolewa – atakupa amani
Okolewa – atakupa ushindi
Alikuja hapa kwa ajili yako.

2. Mbona wewe umepotelea dhambini,
Alikufa mtini kwa ajili yako,
Na Yesuu, ndiye mkombozi,
Atakuokoa ukija kwake.

3. Umechoka sana rohoni mwako,
Unayo mashaka mengi moyoni
Uje kwake Yesu na shida zote,
Aa-anakuita akupumzishe.

4. Nira yake Bwana ni nyepesi mno,
Yeye mnyenyekevu, mpole kabisa,
Na mzigo wake Yesu nimwepesi,
Twendeni kwa Yesu tupate raha.

Chorus x2

4. NINAMTANGAZA MWOKOZI

Ninamtangaza Mwokozi
Kwani yeye ndiye mwema
Hapana mwingine kote
Yeye ndiye namba moja. X2

1. Na vipofu wanaona,
Visiwi wanasikia,
Viwete wanatembea,
Anaweza mambo yote.
Chorus (1)

2. Anaokoa watoto,
Anaokoa vijana,
Anaokoa wazee,
Mkombozi wa watu wote.
Chorus (1)

3. Dunia hii ni maua,
Kama yale yananyauka,
Kila kitu kitapita,
Lakini Yesu atadumu.
Chorus (1)

4. Na Yesu ndiye Mchunga,
Mwalimu tena Kuhani,
Ndiye Mwanzo hata Mwisho,
Njia ya kwenda kwa Baba.
Chorus (x2)

5. BINADAMU HATOSHEKI

1. Binadamu hatosheki, hata awe na mali,
   Na shughuli za kila siku, zamfanya amsahau Mungu.

Binadamu hutosheka akiwa ndani ya Yesu,
Kwani hakuna chochote,
Kitamtenganisha na Bwana.

2. Watu-u wengi duniani, wamelemewa na ulevi,
   Ulafi na usherati, wanapotafuta raha.

3. Kuumbukeni Yudasi, alitaka awe na pesa,
   Akamu-uza Yesu (lakini) hakuipata raha.

4. Tajiri alitamani, awe na maisha mema,
   Na-alipo yapata akamsahau Mungu.

5. Utaf'teni ufalme, na haki ya mbinguni,
   Namahitaji mengine, mtayazidishiwa.

Binadamu hutosheka akiwa ndani ya Yesu,
Kwani hakuna chochote,
Kitamtenganisha na Bwana. X2

6. DAMU YA BARAKA

1. Damu hiyo, ya baraka ituoshayo wakosa; kwake Bwana twaokoka, sasa nasi twaisifu. X 2
   Nimestahili hukumu, siwezi kujitakasa, nioshe katika damu, Takuwa safi kabisa.
   Kabisaaa, kabisa, Nioshe katika damu,
   Takuwa safi kabisa. Takuwa safi kabisa.

2. Yesu alivikwa miiba, nakuangikwa mtini, na maumivu si haba, yaliyompata chini. X2
   Nataka kijito hicho niende kuoga sasa, ndicho kinitakasacho, Nami nisafi kabisa.
   Kabisaaa, kabisa, Ndicho kinitakasacho,
   Nami ni safi kabisa. Nami ni safi kabisa.

3. Baba, kweli nimekosa, moyo wangu ni dhaifu; dhambi ni nyingi Kabisa, nipate wapi wokovu. X 2
   Yesu kijitoni pako naja naamini sasa, Nioshe kwa damu yako, Takuwa safi kabisa.
   Kabisaaa, kabisa, Nioshe kwa damu yako
   Takuwa safi kabisa. Takuwa safi kabisa.

   Kabisaaa, kabisa,
   Nioshe katika damu,
   Takuwa safi kabisa.
   Takuwa safi kabisa.

7. UPEPO UNAPOVUMA

1. Upepo unapovuma naita Yesu,
   Vita vikiwa vikali Yesu haniachi. X2

(Yesu) – Yesu ninaye hataniacha
Kama anipendavyo hataniacha. X2

2. Bwana ananisaidia si-taogopa
   Mwanadamu atende nini si-taogopa. X2

3. Wanaomwamini Yesu, atawabariki,
   Wataipokea taji isiyokauka. X2

4. Anipenda sana sana ananiongoza,
   Aniokoa kabisa, Mwoko-zi mkuu. X2

5. Yeye ndiye jana, leo, ha-ta milele
   Hatabadilika Mungu, ye-ye ni mkuu. X2

(Yesu) – Yesu ninaye hataniacha
Kama anipendavyo hataniacha. X4

8. TUNYENYEKEE MBELE YA MUNGU

1. Yule anavumilia majaribu,
   Amebarikiwa na Mwenyezi Mungu
   Ataipokea taji ya uzima
   Ile Bwana Yesu ametuahidi.

   Tunyenyekee mbele ya Mungu,
   Naye Mungu Baba atatuinua,
   Tunyenyekee mbele ya Mungu,
   Naye Mungu Baba atatuinua.

2. Ewe ndugu yangu unapojaribiwa,
   Usiseme ni Mungu amekujaribu,
   Yeye hawezi kushikana na maovu,
   Walamwenyewe hamjaribu mtu.

3. Kila kitolewacho kilicho kamili,
   Hutoka juu, hushuka kwa Baba wetu,
   Kwake kamwe hakuna kubadilika,
   Wala kivuli cha kugeukageuka.

   Modulate

4. Kwa hivyo wacheni dhambi zote,
   Na kupokea neno lakuwaokoa,
   Tukisikia neno pia tulitende,
   Naye Mungu Baba atatubariki.
   Chorus x2

9. JINA LAKE

1. Jina lake Imanueli (Imanueli) x4
   (Aokoa, anaponya, Mungu pamoja na wanadamu) x2

2. Bwana Yesu ni mshindi (ni Mshiindi) x4
   (Akashinda kifo na mauti, Bwana Yesu, ndiyee mshindi) x2

3. Yesu ni maji ya uzima (ya uzima) x4
   (Yabubujika yaliyo hai, njoni muonje yaliyohai) x2

4. Nguvu zake za ajabu (za ajabu) x 4
   (Damu yake itakusafisha na roho wake atakujaza) x2

5. Tumabalozi wa Yesu (wake Yesu) x4
   (Mabalozi wa Yesu kulitangaza neno lake Bwana) x2

6. Toa vyote kwake Yesu (kwake Yesu) x4
   (Elimu yako na mali yako, Toa vyote kwake Bwana Yesu) x2.

   (Elimu yako na mali yako, Toa vyote kwake Bwana Yesu) x2.

10. KUAMINI BWANA YESU

1. Kuamini Bwana Yesu,
   Kwangu tamu kabisa,
   Kukubali neno lake,
   Nina raha moyoni.

   Yesu, Yesu namwamini, Nimemwona Mwokozi,
   Yesu, Yesu ni rafiki, Ahadi zake kweli. X2

2. Kuamini Bwana Yesu,
   Kwangu tamu kabisa,
   Baraka zake ni nyingi,
   Zafurahisha mioyo.

3. Kuamini Bwana Yesu,
   Kwangu tamu kabisa,
   Hakuna mwingine mwema,
   Wakutuhurumia.

4. Kuamini Bwana Yesu,
   Kwangu tamu kabisa,
   Sipati patanishwa,
   Bila damu yake Yesu.

5. Nashukuru kwa sababu,
   Nimeamini Yesu,
   Mlinzi wa roho yangu,
   Uwe nami daima.
   Chorus x4

11. NANIKIWAZA MOYONI MWANGU

1. Nanikiwaza moyoni mwangu,
Dhambi zile nimeshazitenda,
Naona haya kumuacha mwokozi,
Kwani ameokoa roho yangu.

Naye Yesu atakapowaokoa,
Mtakuwa huru, huru ka – bisa x2

2. Kila atendaye dhambi nimtumwa,
Wala mtumwa hakai nyumbani,
Hurandaranda mahali popote,
Akitafuta pale atapata raha.

3. Hebu kumbuka alivyoteseka,
Msalabani kwa ajili yetu,
Kapigwapigwa mijeledi Yesu,
Ili tupate samaha na uzima.

4. Yesu akasema ndiye wokovu,
Atwokoaye kutoka dhambini,
Kama siyeye tungepotea,
Kwake Mungu akatupokea.

Naye Yesu atakapowaokoa,
Mtakuwa huru, huru ka – bisa x4

12. MWOKOZI WANGU

1. Mwokozi wangu mimi nakupenda,
   Ulimwaga damu ya dhamani,
   Ukafa mtini ili niokoke,
   Nipate uzima milele daima.

2. Yesu mzabibu sisi ni matawi,
   Tuwe ndani yake naye ndani yetu,
   Pasipo Mwokozi hatuwezi kamwe,
   Yeye ndiye mzabibu wa kweli.

3. Ninyi mtalia na ku-omboleza,
   Bali ulimwengu utafurahia,
   Mtahuzunishwa lakini huzuni,
   Utageuzwa na kuwa furaha.

4. Tukikaa ndani yake Bwana Yesu,
   Na neno lake likae ndani yetu
   Chochote tuombacho kwa jina lake
   Tutapewa furaha timilifu.

5. Walakini mimi si peke yangu,
   Kwa kuwa Baba yupo pamoja nami,
   Hapa ulimwenguni kunayo dhiki,
   Lakini jipeni moyo tutashinda.

Na kanisa – Jipeni moyo tutashinda
Wateule - "
Wadada - "
Wandugu - "
Jipeni moyo tutashinda.